Kioo Cha Nafsi

na

Ellis P. Forsman

Kioo Cha Nafsi

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Kioo Cha Nafsi

Yakobo 1:22-24

Yak. 1:22-24, "*Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji tu wala si mtendaji mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo.*"

Watu mara nyingi huvutiwa na kioo, na wengi wetu tunazitumia mara nyingi kwa siku.

Labda, hata mtumwa alivutiwa katika kujitazama katika visima au mabwawa ya maji katika wakti wake.

Wanadamu wamefanya aina tofauti tofauti za vioo, hata kuangalia sehemu ambazo ni vigumu kuangalia kwa kawaida.

Mungu ametengeneza kioo ambayo umulika nafsi ya mwanadamu.

Hii inatajwa kuonyesha umuhimu wa kuwa watendaji wa neno. Imekusudiwa kuonyesha kwamba Biblia ndiyo kiwango cha kumwonyesha mwanadamu njia.

Kioo kinaonyesha kile kinachohitaji marekebisho.

Vioo havina ukamilifu

Vioo vianvyotengenezwa na wanadamu vina kasoro. Baadhi ya hizi utengenezwa hivyo kwa malengo ya kuonyesha kuumbuka, kama mtu akiikuta katika nyumba ya maonyesho.

Lakini neno la Mungu, ambayo ndiyo kioo cha nafsi, haionyeshi picha ya kuumbuka. Ni kamilifu.

Yak. 1:25, "*Lakini aliyeitazama sheria kanilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*"

Kusudi la kioo

Kusudi la kioo, kimsingi, ni kufunua – kutoa mtazamo mzuri. Kioo kinasema jinsi ilivyo, nzuri au mbaya.

Kama marekebisho yanatakiwa kufanywa, ye yote anayejiangalia kwenye kioo, lazima afanye marekebisho.

Neno la Mungu ndio kioo cha nafsi (Yakobo 1:22-24, hapo juu).

Inaiambia jinsi ilivyo. Kile inachosema maranyingi sio picha inayopendeza.

Kujitazama sisi wenyewe katika kioo haitubadilishi. Kubadilika, lazima tufanye kile ambacho Mungu anatuambia. (Yakobo 1:22-24, hapo juu).

Sawa na kioo ya kimwili, marekebisho lazima yafanywe na mtu binafsi, kama jinsi neno linavyosaidia katika kufunua.

Kama tukiona kutokukamilika kwetu jinsi tunavyoangalia katika neno, alafu tusifanye cho chote kuyarekebisha, sisi ni sawa na mtu anayejitazama mwenyewe katika kioo, alafu asifanye cho chote juu yake. Kioo hakimsaidii, na neno la Mungu haitusaidii chini ya hali kama hiyo.

Neno la Mungu linafunua vitu vingi

Neno la Mungu, kioo cha nafsi, inaonyesha ulikotoka unapoitazama.

- Mwanzo 1:26, "*Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu …*"
- Mwanzo 2:7, "*BWANA Mungu akafanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.*"

Katika kioo hiki unaweza kuona ya kuwa wewe sio nyani.

Kioo cha Mungu hufunua matendo yako.

Sawa na jinsi chakula kikianguka kwenye tai kinaweza kufunua kile ulichokula, au urembo ambao wanawake hupaka mdomoni kuweka doa katika ukosi wa nguo yako inafunua kile ulichokuwa unakifanya, neno la Mungu hufunua aina ya mtu alivyo.

- Rum. 3:23, "*Kwa sababu wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;*"
- 1 Yoh. 3:4, "*Kila atendaye dhambi afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi.*"
- Gal. 5: 19-21, "*Basi matendo ya mwili ni dhahiri ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.*"

Kioo cha Mungu ufunua mahitaji yako.

Sawa na jinsi kioo chako cha kimwili kinaweza kufunua kwamba unahitajika kuosha uso wako.

- Rum. 5:8-10, "*Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye. Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baad ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake.*"
- Rum. 1:16-17, "*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.*"
- Fil. 2:12-13, "*Basi wapendwa wangu, kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo, bali sasa zaidi mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.*"

Kioo cha Mungu ufunua hitimisho lako.

Kama jinsi kioo chako cha kimwili kinavyoweza kuonyesha jinsi ulivyovaa kwamba unajiandaa kufanya kazi bustanini, ukihusika katika michezo, kwenda sehemu tofauti tofauti, au kwenda kanisani.

Yoh. 5:28-29, "*Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.*"

Kioo cha Mungu kinatuambia kwamba ni wakati wetu wa kuwa na mtazamo mzuri.

Sasa, kioo chako cha kimwili hakikuiti, ikisema, "Hei, fulani, kweli unataka kuvaa shati hilo na nguo hizo?"

Lakini kioo cha Mungu hakika utuonyesha kwamba ni afadhali tujijaribu sisi wenyewe.

2 Kor. 13:5, "*Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa.*"

Usiichukie kioo

Watu hawaichukii kioo, bila kujali upungufu inayoonyesha.

Waenda kanisani wanaweza kuwa na tabia sawa na hizi wanapoona kile ambacho hawakipendi katika kioo cha Mungu. Kwa nini uichukie kioo cha Mungu? Mwenye dhambi wakati fulani anamchukia Mungu, au mtu anayeshikilia kioo chake mbele yetu.

- Zaburi 14:1, "*Mpumbavu amesema moyoni, hakuna Mungu; wameharibu matendo yao na kuyafanya chukizo, hakuna atendaye mema.*"
- 2 Thes. 1:7-9, "*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoangamizwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake.*"

Ni mewahi kusikia mwenye dhambi mpitaji akikataa ubatizo kama sehemu ya wokovu wa Mungu kwa mwanadamu; au mwingine anachukia anapoonyeshwa kile anacho kifanya, Mungu anasema ni dhambi.

Tito 2:11-14, "*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema.*"

Matumizi sahihi ya neno la Mungu ni muhimu

Ipaswa itumiwe kwa kutii.

Yak. 1:22-25, "*Lakini iweni watendaji wa neno wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru na kuka humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*"

Inatakiwa itumiwe mara zote na kila mara.

Zab. 1:1-2, "*Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya BWANA ndiyo ipendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku.*"

Lazima itumiwe kwa halali na uwazi.

Mdo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

Hitimisho

Je unatazama katika kioo cha nafsi yako? Itakuonyesha hakika jinsi ulivyo.

Kama bado wewe siyo Mkristo, kioo cha Mungu kitakwambia ni jinsi gani. Kuna hatua ambazo unatakiwa kuzifuata:

Imani.

- Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"
- Yoh. 12:46, "*Mimi nimekuja ili niwe nuru ya ulimwengu, ili kila mtu aniaminiye mimi asikae gizani.*"
- Rum. 10:9, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.*"

Toba.

- Mdo. 17:30, "*Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.*"
- Luka 13:3, "*Nawaambia sivyo; lakini msipotubu ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.*"
- Mdo. 3:19, "*Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana.*"

Kukiri.

- Fil. 2:11, "*Na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba.*"
- Mt. 10:32, "*Basi kila mtu atakayenikiri mbele ya watu nami nitamkiri mbele ya Baba yangu aliyembinguni.*"
- Rum. 10:9, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.*"

Ubatizo.

Mt. 28:19, "*Basi enendeni mkayafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu;*"

Yoh. 3:5, "*Yesu akajibu, Amini, amini, nakuambia mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*"

Mk. 16:16, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa.*"

Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Mdo. 22:16, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*"